



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU UBORESHAJI WA
MAJARIBIO WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA**

Dodoma, 10 Novemba, 2023

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya zoezi la uboreshaji wa majaribio wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika Kata ya Ng'ambo iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, Mkoa wa Tabora na Kata ya Ikoma iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, Mkoa wa Mara kuanzia tarehe 24 hadi 30 Novemba, 2023.

Zoezi la uboreshaji wa majaribio utafanyika katika vituo 16 vya kuandikisha wapiga kura. Kati ya hivyo, vituo 10 ni vya Kata ya Ng'ambo na vituo sita (6) vipo Kata ya Ikoma. Vituo vya uandikishaji vitafunguliwa saa 2:00 asubuhi na kufungwa saa 12:00 jioni.

Zoezi hili linafanyika kwa lengo la kupima uwezo wa vifaa na mifumo ya uandikishaji itakayotumika wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura unaotarajiwa kufanyika nchi nzima kwa tarehe na ratiba itakayopangwa na Tume.

Uboreshaji wa majaribio utahusisha kuandikisha raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi na atakayetimiza umri wa miaka 18 kabla au ifikapo tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, wapiga kura wanaoboresha taarifa zao ambao wamehama kutoka eneo moja la uchaguzi kwenda eneo jingine, waliopoteza au kadi zilizoharibika, wanaorekebisha taarifa zao na kuondoa wapiga kura waliopoteza sifa za kuwemo katika Daftari.

Katika zoezi hilo, Tume itatumia *BVR Kits* zenye vifaa mbalimbali vinavyowasiliana ili kuchukua na kutunza taarifa za wapiga kura. *BVR Kits* hizo zimeboreshwa na ni tofauti na zile zilizotumika katika zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mwaka 2015 na 2019.

Aidha, Tume imesanifu na kuboresha mfumo wa uandikishaji wa Wapiga Kura (Voters Registration System-VRS) ili kukidhi muundo na *BVR Kits* za sasa ambazo zinatumia programu ya *android* tofauti na *BVR Kits* za awali ambazo zilikuwa zinatumia programu ya *Microsoft Windows*.

Mfumo wa uandikishaji ulioboreshwa utawawezesha wapiga kura ambao wameshaandikishwa na wapo kwenye daftari la wapiga kura, kuanzisha mchakato wa kuboresha taarifa zao ama kwa kubadilisha kituo cha kupigia kura iwapo amehama Mkoa au Wilaya nyingine au kurekebisha taarifa zao kwa njia ya mtandao kwa kutumia simu zao za mkononi au kompyuta.

Kuanzisha mchakato mtandaoni, mpiga kura ataingia kwenye tovuti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi www.nec.go.tz kwa kutumia kompyuta au simu janja kisha atabonyeza kiunganishi (link) kilichoandikwa “Boresha Taarifa za Mpiga Kura” au atatumia anuani ya ovrs.nec.go.tz itakayompeleka moja kwa moja kuanzisha mchakato. Baada ya kufuata utaratibu huo, mfumo utamletea ukurasa wenye vipengele vitakavyomruhusu kuweka taarifa zake kulingana na mahitaji.


Baada ya kukamilisha taratibu zote na kuwasilisha taarifa kwenye mfumo, mpiga kura atapokea ujumbe mfupi wenye kumbukumbu namba kupitia namba yake ya simu aliyoitumia wakati wa kuboresha taarifa zake kwenye mtandao. Kumbukumbu namba hiyo atakwenda nayo kwenye kituo cha kuandikisha wapiga kura kwa ajili ya kumalizia hatua zilizobaki na kupatiwa kadi.

Katika uboreshaji huu wa majaribio, vyama vya siasa vitashiriki kwa kuweka wakala mmoja katika kila kituo cha kuandikisha wapiga kura, lengo ni kushuhudia na kujiridhisha kuhusu taratibu zitakazotumika wakati wa uboreshaji wa majaribio wa Daftari.

Utaratibu ulioainishwa wa kuboresha taarifa kwa njia ya mtandao, hautawahusu wapiga kura wanaotaka kuandikishwa kwa mara ya kwanza na wapiga kura ambao kadi zao zimeharibika au kupotea. Hawa wanashauriwa wafike kwenye kituo cha kuandikisha wapiga kura na kufuata taratibu watakazoelekezwa na Maafisa wa Tume watakaokuwepo kwenye kituo.

Tume inatoa wito kwa wananchi wenye sifa zilizotajwa wa Kata ya Ng'ambo iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na Kata ya Ikoma iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, kujitokeza kwa wingi kushiriki katika uboreshaji wa majaribio wa Daftari na kutoa ushirikiano kwa Tume wakati wote wa utekelezaji wa jukumu hili muhimu kwa mustakabali wa Taifa.

Imetolewa na:



Kailima, R. K

MKURUGENZI WA UCHAGUZI